


Kwa kila mistari hii mitatu ni nini lazima tunafanya na tutakua nini?

“Bali wote WALIOMPOKEA aliwapa uwezo wa kufanyika WATOTO WA MUNGU.” Yohana 1:12

“Kwa kuwa, kila ATAKAYELITIA jina la Bwana ATAOKOKA.” Warumi 10:13

“Yeye aliye naye MWANA anao huo UZIMA;  
ASIYE NAYE MWANA WA MUNGU HANA HUO UZIMA. . . .  
ILI MJUE ja kuwa mna UZIMA WA MILELE” I Yohana 5:12,13



“Amini amini, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; Wala haingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.” Yohana 5:24

DAI KARMA ya uzima wa milele kwa kumpokea Kristo kama MWOKOZI wako, ukimwambia mungu kitu kama hiki:

- Mungu mwenyezi nimekuwa kinyume kwako, nikitenda dhambi kwa fikira, maneno na kwa matendo. Nimesikitika kwa hii na ninataka Yesu Kristo anisamehe dhambi zangu zote.
- Mimi sasa NINAKUPOKEA wewe BWANA YESU KRISTO kama MWOKOZI wangu na MUNGU wangu, na sasa NINAKUOMBA WEWE BWANA YESU hili
  - UNIPOKEA KUTOKA KWA DHAMBI ZANGU NA ZIWA LA MOTO.
  - UNICHUKUE MBINGUNI WAKATI NITAKUFA, na
  - UNIPUKEA KWA UZIMA WA MILELE sasa hivi.
- UZIMA WANGU KWAKO WEWE BWANA YESU UINGIE NDANI UE MWOKOZI WANGU, na RAFIKI YANGU, na MUNGU wangu, milele katika jina la Yesu, Amini.

Sahihii: ..... Tarehe: .....

“Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe.” Yohana 10:28

“Kama ukikiri kwa kinywa chako kuwa Yesu ni Bwana na ukiamini moyoni mwako kuwa Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka” Warumi 10:9

**LIBERTY BAPTIST CHURCH**, PO Box 188, Cherrybrook NSW 2126. Ph (+61 2) 9875 4321.  
Kiswahili [www.keithpiper.org](http://www.keithpiper.org) [www.libertybaptistchurch.org.au](http://www.libertybaptistchurch.org.au)  
Youtube, Answers Course, Lesson 7.

# SIMAMA!




KARAMA YA  
MUNGU  
NI UZIMA WA  
MILELE!

JE WEWE  
UMEUPOKEA?


Tutaweza je kuwa na UKWELI ya kwamba tuko na UZIMA WA MILELE? Ni lazima TUJUE vitu vinne (4):

## 1. WOTE WAMEFANYA DHAMBI


"KWA SABABU WOTE WAMEFANYA, DHAMBI, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Warumi 3:23



Kujitangulize



Kuachana na Mungu



Kupungukiwa na ukamilifu kawaida wa Mungu

1. Usiwe na miungu mingine.
2. Usijifanyie sanamo ya kuchonga.
3. Usilitaje bure jina la Bwana.
4. Ikumbuke siku ja Sabato uitakase.
5. Waheshimu baba yako na mama yako.

6. Usiue.
7. Usizini.
8. Usiibe.
9. Usimshuhudie jirani yako uongo.
10. Usitamani nyumba ya jirani yako.

Dhambi ni kutotii amri za Mungu - Biblia

Sisi ni wenye DHAMBI WAKUU tukilinganishwa na UTAKATIFU WA MUNGU.

Q1: Ye! unataka Mungu wa Biblia awe Mungu wako?

Q2: Je! unataka ukome kwa dhambi na uje kwa Mungu? (Toba)

## 2. MALIPO YA DHAMBI NI MAUTI

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni MAUTI bali KARAMA YA MUNGU ni UZIMA WA MILELE katika Kristo Yesu Bwana wetu." Warumi 6:23

"MAUTI na KUZIMU zikatupwa katika lile ZIWA LA MOTO. Hii ndiyo MAUTI YA PILI." Ufunuo wa Yohana 20:14

**Maelezo:** Kwa sababu sisi zote tumefanya.

**Dhambi:** Amri za Mungu zinasema, sisi zote tunaangalia kifo na tutatupwa katika ziwa la moto. Hii ni habari mbaya sana. Wewe na mimi hatutaki kwenda kwa ziwa la moto.

Tuna njia yeyote itatusaidia? Ndiyo!

Mungu anatutolea, toleo ya Uzima wa milele tunapata katika Kristo Yesu, si kwa sababu ya kazi yetu nzuri, ama dhehebu lolote.

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; WALA SI KWA MATENDO, mtu awaye yote asije akajisifu." Waefeso 2:8,9

Zawadi ni toleo la bure. Utachukua au uwache Maana ya uzima wa milele ni kumjua Mungu, na kuenda mbinguni baada ya kifo. Kwa hivyo AMRI za Mungu zinasema tutaenda kwa ziwa la moto, lakini UPENDO wa Mungu, unatushahili twende mbinguni. Angalia vile Mungu ametutolea kusamehewa bure na uzima wa milele.

...Mauti nii:



Wakati miili yetu inakufa



Ukifungua ukurasa mpya haufuti ya samani




## 3. KRISTO YESU ALICHUKUA ADHABU YETE YOTE

"Bai Mungu aonyesha PENDO lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa KRISTO ALIKUFA KWA AJILI YETU, tuilipokuwa tungali WENYE DHAMBI." Warumi 5:8

"Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote" Isaya 53:6

Yesu ni MWOKOZI wa WATU WOTE yeye sasa ANAWEZA kuwa MWOKOZI WAKO.

Dhambi za kila mtu zilizopita na za mbele.



Angalia: Mungu alichukua dhambi zote za kale sasa na za mbele KUTOKA KWETU na akaziweka JUU ya KRISTO.

Yesu alichukua ADHABU KAMILI ya dhambi zetu SOTE juu msalabani, badala yetu kuhukumiwa milele katika ziwa la moto.


Yesu sasa ni MWOKOZI (mchukua – dhambi) wa watu WOTE MILANGO kuingi mbinguni sasa uko wasi kwa WOTE waingie. Lakini TUTAWEZAJE kuingia mbinguni?

### 4. (a) AMINI YA kwamba YESU KRISTO

- ni MUNGU MWANA (100% Mungu na 100% Mwanadamu)
- ALIKUFA KWA AJILI YETU
- ALIFUFUKA KUTOKA kwa WAFU NA MWILI, halafu

### (b) WAMEMUPOKEA YESU KRISTO kama MWOKOZI wao

WAMESAMEHEWA BURE na wamepewa UZIMA WA MILELE sasa hivi. Hii inamaanisha ya kwamba, sasa umekubari dhabihu ya damu ya Yesu Kristo juu msarabani kama malipo kamili ya dhambi zako, kumwamini Yesu pekee akuokoe, sio kazi yako nzuri au dini yeyote.



Tuna HAKIKA ya haya kwa sababu ya ahadi ya Mungu alitukabidhi tujidai katika Biblia: